

MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA



TAARIFA YA UTENDAJI KAZI YA MWAKA 2017/18

BARUA YA KUWASILISHA



Mhe.Ummy A. Mwalimu (MB),
Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii,
Jinsia, Wazee na Watoto,
Chuo kikuu cha Dodoma,
Kitivo cha Sanaa ya Sayansi ya
Maendeleo ya jamii, Jengo Na 11
S.L.P 743,
404780 Dodoma



Dkt. Mpoki M.Ulisubisya,
Katibu Mkuu - Afya,
Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii,
Jinsia, Wazee na Watoto,
Kitivo cha Sanaa ya Sayansi ya
Maendeleo ya Jamii, Jengo Na 11
S.L.P 743,
404780 Dodoma

Mhe. Waziri,

Ninayo heshima kubwa kuwasilisha kwako Taarifa ya Utendaji Kazi ya Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) kwa kipindi cha mwaka 2017/18.

Taarifa hii imeeleza utekelezaji wa shughuli za Mamlaka katika kutimiza lengo lake kuu la Kulinda Afya ya Jamii kwa kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi.

Nawasilisha.

A handwritten signature in black ink, appearing to read "Mpoki".

**Dkt. Mpoki M. Ulisubisya
Katibu Mkuu (Afya)**

MAELEZO YA MWENYEKITI WA BODI YA USHAURI (MAB)

Taarifa ya utendaji kwa mwaka wa fedha 2017/18 inaainisha kazi na majukumu yaliyotekelizwa na Mamlaka katika kipindi husika pamoja na maeneo yanayohitaji kupewa kupaumbele katika mwaka ujao wa fedha ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Huu ni mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango mkakati wa miaka mitano (5) wa TFDA wa 2017/18 – 2021/22 ambaa umelenga kuimarisha utekelezaji wa jukumu la msingi la kulinda afya ya jamii kwa kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi.

Mamlaka imeendelea Kuboresha huduma zake kwa wateja kwa kutumia TEHAMA na kutekeleza mifumo bora ya kiutendaji (Quality Management System) kwa kiwango cha kimataifa cha ISO 9001:2015 katika kutoa huduma.

TFDA imewekeza katika ununuzi wa vifaa vya kisasa vya maabara na kuwajengea uwezo wachunguzi pamoja na kukamilisha ujenzi wa maabara ya Kanda ya Ziwa, Mwanza ambayo imesogezza huduma karibu na wananchi. Aidha, maabara ya Chakula na ya Maikrobiolojia zimeendelea

kushikilia cheti cha ithibati (accreditation) kwa kiwango cha Kimataifa cha ISO/IEC 17025:2015 baada ya kukaguliwa tena (surveillance) na taasisi za ithibati za SADCAS/SANNAS. Hii inafanya matokeo ya chunguzi zinazofanywa na maabara za TFDA kuendelea kutambuliwa kimataifa.

Utekelezaji wa majukumu na utoaji huduma umezingatia Sheria, Kanuni na taratibu pamoja na matumizi sahihi ya rasilimali ambapo hesabu za fedha na rasilimali za TFDA kwa kipindi kinachoishia Juni, 2018 zipo kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa ajili ya ukaguzi. Vilevile, hesabu za fedha na rasilimali kwa kipindi kinachoishia Juni 2017 zilikaguliwa na TFDA kupata hati safi kwa mwaka wa 11 mfululizo.

Kwa ujumla, kumekuwa na mafanikio makubwa katika utekelezaji wa majukumu yake ambapo bidhaa zilizosajiliwa, maeneo yaliyokaguliwa, idadi ya sampuli zilizochunguzwa kimaabara pamoja maeneo ya kufanya biashara yaliyosajiliwa na Mamlaka kwa mwaka 2017/18 imeongezeka ikilinganishwa na mwaka uliopita. Pamoja na mambo mengine, mafanikio haya yamechangiwa na kuongezeka

kwa idadi ya watumishi, vitendea kazi, mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi, mwamko wa wafanyabiashara pamoja na elimu kwa umma.

Naipongeza Menejimenti pamoja na wafanyakazi wote wa TFDA kwa kufanya kazi kwa weledi na kujituma katika kuhakikisha kuwa bidhaa. Vilevile, natoa shukrani kwa wadau wote wa Mamlaka ikiwa ni pamoja na jamii kwa ujumla kwa ushirikiano wao katika kusaidia Mamlaka kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Aidha, natoa wito kwa wadau wote wa TFDA na wananchi kwa ujumla kutekeleza wajibu wao ipasavyo katkia kuhakikisha kuwa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi vilivyopo katika soko vinakidhi vigezo vya ubora na usalama.



**Balozi Dkt. Ben Moses
MWENYEKITI WA BODI YA
USHAURI (MAB)**

MAELEZO YA MKURUGENZI MKUU

Mamlaka ya Chakula na Dawa –TFDA in a a d h i m i s h a miaka 15 tangu ilipoanza kutekeleza majukumu yake rasmi tarehe 01 Julai, 2003. Pamoja na kufikia malengo iliyojiwekea katika kulinda afya ya jamii kwa kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi, Mamlaka imekumbwa na changamoto mbalimbali katika kipindi hicho.

Taarifa ya utendaji kazi ya TFDA kwa mwaka wa fedha 2017/18 inaanisha majukumu na kazi zilizofanyika katika kipindi tajwa. Aidha, changamoto zilizojitokeza pamoja na mbinu zilizotumika kuzikabili zimeanishwa.

Hivi sasa Mamlaka inatekeleza mpango mkakati wa miaka mitano (2017/18 - 2021/22) ambao umejikita katika kutekeleza malengo mkakati Nane (8) ambayo ni; Kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi; Kuhakikisha usalama na ubora wa chakula; Kuboresha huduma za maabar; Kuimarisha utoaji elimu kwa umma na kuboresha huduma kwa wateja; Kuimarisha

uwezo wa Mamlaka katika kutoa huduma za udhibiti; Kupunguza maambukizi ya virusi vyta UKIMWI na kuboresha huduma kwa waathirika wa UKIMWI na magonjwa yasiyoambukiza; Kuimarisha na kutekeleza kwa ufanisi Mkakati wa Taifa wa kupambana na kuzuia rushwa; na Kuboresha masuala ya jinsia na mazingira. Hatua ya utekelezaji wake imezingatiwa katika taarifa hii.

Kumekuwa na mafanikio makubwa katika Kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi ambapo jumla ya maombi 3,762 ya usajili wa dawa vipodozi, vifaa tiba, vitendanishi na vipukusi yalipokelewa na 3,571 kati ya hayo sawa na 95% yalitathminiwa ambapo 2,161 (61%) yaliidhinishwa. Aidha, maombi 4,894 ya usajili wa maeneo ya biashara ya dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi yalipokelewa na kutathminiwa ambapo maombi 4,731 (96.67%) yaliidhinishwa idadi ya maombi yalijotathminiwa imeongezeka kutoka 3,535 mwaka 2016/17 mpaka 4,894 sawa na ongezeko la 38% huku idadi ya maeneo yaliyokidhi vigezo yakiongezeka kutoka

maeneo 3,319 mwaka 2016/17 hadi 4,730 .

Katika kuhakikisha usalama na ubora wa chakula, maombi 2,571 ya usajili wa chakula ikiwa ni ongezeko la maombi 417 sawa na asilimia 20 ya maombi ya mwaka 2016/17 yaliyopokelewa na kati yake maombi 2,329 sawa na 91% yalitathminiwa na maombi 2,104 yaliidhinishwa. Pia, maombi 6,767 ya usajili wa maeneo ya biashara ya chakula yalipokelewa. Maombi haya ni ongezeko la maeneo 653 (11%) ikilinganishwa na maombi 9,320 yaliyotathminiwa mwaka 2016/17 na kati yake maombi 6,723 sawa na 99% yalitathminiwa na kati yake maombi 6,294 (94%) yalikidhi vigezo. Mwaka huu kuna ongezeko la maeneo 1,411 (43%) ikilinganishwa na maeneo 3,319 yaliyosajiliwa mwaka 2016/17.

Katika usajili wa maeneo jumla ya maeneo 9,277 ya biashara ya dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi yaliyokaguliwa ambapo maeneo 7,607 (82%) yalikidhi vigezo. Hii ni ongezeko la 20% ikilinganishwa na maeneo 6,332 yaliyokaguliwa mwaka 2016/17. Aidha maeneo 10,273 yanayojihusisha na biashara

ya chakula yalikaguliwa na maeneo 7,093(69) kati yake yalikidhi vigezo. Idadi ya maoneo yanayojihuisha na biashara ya chakula ni ongezeko la maeneo 953 (10%) ikilinganishwa na maeneo 9,320 yaliyokaguliwa mwaka 2016/17. Vilevile wastani wa kukidhi vigezo kwa maeneo yanayojihuisha na biashara ya chakula yaliyokaguliwa umeongezeka kutoka 65% kwa mwaka 2016 / 17 hadi 69%.

Katika kipindi hiki jumla ya sampuli 5,855 zilipokelewa kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara na 5,165 (88%) zilichunguzwa ambapo 4,358 (84%) zilifaulu. Aidha, katika kuhakikisha kwamba viwango vya ISO / IEC 17025:2005 na WHO / GLP vinafuatwa na kutekelezwa, Mamlaka ilihuisha ithibati ya umahiri wa uchunguzi kwa maabara za Chakula pamoja na Maikrobailojia na hivyo kupewa vyeti vya Ithibati kwa kipindi kingine cha miaka mitano (5) kuanzia Februari 2018 hadi Februari 2023.

Katika kuimarisha utoaji Elimu kwa Umma na kuboresha huduma kwa wateja, elimu ilitolewa kwa makundi ya wadau kuitia njia mbalimbali za uelimishaji ambazo ni

pamoja na kufanya mihadhara ya wazi 136 kwa wananchi 65,753, kurusha matangazo mafupi ya uelimishaji kuitia vipindi vya runinga na radio na kushiriki katika maonesho.

Kwa upande wa usimamizi wa rasilimali fedha, Mamlaka ilikusanya jumla ya TZS 49.8 bilioni ambapo asilimia themanini (80%) zilitokana na ada na tozo, 3.8 bilioni (8%) ni kutoka Serikali kuu na TZS 6 bilioni (12%) ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Aidha, asilimia (96%) zilitumika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Mamlaka kwa mujibu wa Mpango kazi na Bajeti kwa mwaka 2017 / 18.

Kwa ujumla Mamlaka ilitekeleza kwa ufanisi majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Mpango Kazi na Bajeti wa 2017/18 na hivyo kufikia na kuvuka malengo iliyojiwekea. Aidha, Mamlaka imeweza kusimamia mifumo ambapo imeweza kushikilia Cheti cha ubora wa mifumo cha ISO 9001:2015 na Cheti cha Ithibati ya Mifumo ya Maabara kwa kiwango cha ISO / IEC 17025 :2005 na utambuzi wa WHO.

Katika mwaka wa fedha

2018/19 Mamlaka itatoa kipaumbele katika maeneo ambayo haikufanya vizuri hususan kukamilisha upanuzi wa Maabara ya Makao Makuu, uchunguzi wa sampuli za bidhaa na kuwajengea uwezo wasindikaji wadogo na wa kati ili waweze kufikia vigezo vya usajili wa majengo na bidhaa zao. Vilevile, Mamlaka itaimarisha mfumo wa uwianisho wa vibali vinavyotolewa na shehena zinazokaguliwa katika vituo vya forodha, kuimarisha mifumo ya kielektroniki ili kuongeza huduma zitolewazo kwa njia ya matandao.

Nichukue fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza wafanyakazi wenzangu wa TFDA. Vilevile, natoa shukrani za dhati wa Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi ya ushauri (MAB) kwa maelekezo sahihi yaliyowezesha kufikia mafanikio haya.



.....
Adam M. Fimbo
KAIMU MKURUGENZI
MKUU

JENGO LA TFDA JIJINI MWANZA



TFDA imeendelea kuimarisha Miundombinu na kusogeza huduma karibu zaidi na Wananchi

TAARIFA KAMILI

1.0 Utangulizi

Mamlaka ilianza kutekeleza Mpango Mkakati wake wa nne (4) wa miaka mitano (5) (2017/18 - 2021/22). Taarifa hii inaainisha kazi zilizotekeliza kwa kipindi cha Julai, 2017 – Juni, 2018 kwa kuzingatia Malengo mahususi manane (8) yaliyomo katika Mpango Mkakati kama ilivyoainishwa hapa chini:–

- a) Kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi;
- b) Kuhakikisha usalama na ubora wa chakula;
- c) Kuboresha huduma za maabara;
- d) Kuimarishe utoaji elimu kwa umma na kuboresha huduma kwa wateja;
- e) Kuimarishe uwezo wa Mamlaka katika kutoa huduma za udhibiti;
- f) Kupunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI na kuboresha huduma kwa waathirika wa UKIMWI na magonjwa yasiyoambukiza;
- g) Kuimarishe na kutekeleza kwa ufanisi Mkakati wa Taifa wa kupambana na kuzuia rushwa; na
- h) Kuboresha masuala ya jinsia na mazingira

1.1 Hatua ya Utekelezaji wa kila Lengo Mahsusni

Utekelezaji wa kila lengo mahsusni katika Mpango Mkakati wa miaka mitano (5) wa TFDA umefanyika kama ilivyoainishwa vipengele 1.1.1 hadi 1.1.8.

(a) – (f). Mchanganuo wake umeainishwa katika Jedwali Na.1

(a) Tathmini na usajili wa dawa za binadamu

Jumla ya maombi 1,068 yalipokelewa ambapo 625 ni mapya na 443 ya kuhuisha. Aidha, kulikuwa na baki ya maombi 69, yakiwemo 41 mapya na 28 ya kuhuisha kutoka mwaka wa fedha 2016/17 hivyo kufanya jumla ya maombi yote kuwa 1,137 (666 mapya na 471 kuhuisha). Jumla ya maombi 1,024 (90%) yalifanyiwa tathmini na maombi 738 (72%) yaliidhinishwa.

(b) Tathmini na usajili wa dawa za mifugo

Katika eneo hili jumla ya maombi 86 yalipokelewa yakiwemo 56 mapya na 30 ya kuhuisha. Vile vile hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017, kulikuwa na maombi yaliyobaki saba (7) ambapo matatu (3) yalikuwa mapya na manne (4) ya kuhuisha hivyo kufanya jumla ya maombi yote kuwa 93 ambapo 59 yalikuwa mapya na 34 ya kuhuisha. Kati ya hayo, 88 (95%) yalifanyiwa tathmini na maombi 61

1.1.1 K U H A K I K I S H A USALAMA, UBORA NA UFANISI WA DAWA, VIPODOZI, VIFAA TIBA NA VITENDANISHI

Mojawapo ya jukumu la msingi la Mamlaka ni kuhakikisha kwamba afya ya wananchi inalindwa dhidi ya athari ambazo zinaweza kujitokeza kutokana na matumizi ya dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi kwa kufanya usajili na ukaguzi, kufuatilia madhara yatokanayo na bidhaa zinazodhibitiwa, kufanya ufuatiliaji wa ubora na usalama wa bidhaa husika katika soko. Katika kipindi cha mwaka 2017/18, Mamlaka ilitekeleza kazi kama ilivyoainishwa katika kipengele 1.1.1.1 mpaka 1.1.1.8.

1.1.1.1 Usajili wa dawa, vipodozi, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyongeza

Katika kutekeleza majukumu haya kazi zilizofanyika zinajumuisha tathmini na usajili wa dawa za binadamu, mifugo, vipodozi, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyongeza kama ilivyoolezwa katika vipengele

(69%) yaliidhinishwa.

(c) Tathmini na usajili wa bidhaa nyongeza

Katika kundi hili, jumla ya maombi 75 ya usajili wa vipukusi yalipokelewa ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017 kulikuwa na maombi manne(4) yaliyobaki ya mwezi hivyo kufanya jumla ya maombi yote ya usajili wa bidhaa husika kuwa 79. Maombi yote 79 yalifanyiwa tathmini, 38 yaliidhinishwa na kusajiliwa. Vile vile, ombi moja (1) la usajili wa dawa za mitishamba lilipokelewa na kufanyiwa tathmini.

(d) Tathmini na usajili wa vipodozi

Jumla ya maombi 1,755 ya usajili wa vipodozi yalipokelewa ambapo 1,468 yalikuwa mapya na 287 yakuhisha. Pia kulikuwa na maombi 107 yaliyobakia hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017 ambapo 104 yalikuwa mapya na matatu (3) ya kuhuisha hivyo kufanya jumla ya maombi kuwa 1,862 ambapo maombiyote yalifanyiwa tathmini. Kati ya maombi yaliyofanyiwa tathmini, 1,136 sawa na 61% yaliidhinishwa, 18 yalikataliwa na yaliyobaki yana hoja.

(e) Tathmini na usajili wa

vifaa tiba na vitendanishi

Kulikuwa na jumla ya maombi 575 ambapo 504 yalipokelewa katika kipindi cha 2017/18 na 71 ni baki ya mwaka 2016/17. Maombi 503 sawa na 88% yalifanyiwa tathmini ambapo 179 sawa na 36% yaliidhinishwa.

(f) Tathmini ya Maombi ya Majaribio ya Dawa

Jumla ya maombi 15 ya majaribio ya dawa yalipokelewa ambapo 14 sawa na 93% yalifanyiwa tathmini na maombi nane (8) kati ya maombi yaliyofanyiwa tathmini yaliidhinishwa.


Jedwali Na. 1: Idadi ya maombi ya usajili wa dawa, vipodozi, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyongeza

Na	Aina ya bidhaa	Maelezo	Baki 2016/17	Pokelewa	Jumla	Tathmininiwa	Idhinishwa	Kataliwa	Baki
Dawa	Binadamu	Mapya	41	625	666	599	282	16	67
		Huishwa	28	443	471	425	456	0	46
		Jumla ndogo	69	1,068	1,137	1,024	738	16	113
	Mifugo	Mapya	3	56	59	54	33	3	5
		Huishwa	4	30	34	34	28	-	-
		Jumla ndogo	7	86	93	88	61	3	5
	Mitishamba	Mapya	0	1	1	1	1	0	0
		Huishwa	0	0	0	0	0	0	0
		Jumla ndogo	0	1	1	1	1	0	0
1	Majaribio ya dawa	Mapya	0	15	15	14	8	0	1
2		Jumla ndogo	0	15	15	14	8	0	1

		Mapya	104	1,468	1,572	1,572	918	16	0	
		Huishwa	3	287	290	290	218	2	0	
3	Vipodozi	Jumla ndogo	107	1,755	1,862	1,862	1,136	18	0	
		Mapya	4	75	79	79	38	0	0	
		Huishwa	0	0	0	0	0	0	0	
4	Vipukusi	Jumla ndogo	4	75	79	79	38	0	0	
		Mapya	71	490	561	489	165	3	72	
		Huishwa	0	14	14	14	14	0	0	
5	Vifaa tiba na vitendanishi	Jumla ndogo	71	504	575	503	179	3	72	
		Jumla Kuu		2,58	3,504	3,762	3,571	2,161	40	191

Kwa mujibu wa Jedwali husika hapo juu, kati ya maombi 3,762 yaliyokuwepo, maombi 3,571 (95%) yalifanyiwa tathmini ambapo 2,161 (61%) yaliidhinishwa kama ilivyooneshwa katika mchoro Na.1.

Mchoro Na.1: Mchanganuo wa maombi ya bidhaa yaliyokuwepo, yaliyotathimiwa na yaliyoidhinishwa



(g) Tathmini ya maombi ya matangazo, mabadiliko na majibu ya hoja zinazohusu usajili wa dawa, vipodozi, vifaa tiba na bidhaa nyongeza

Katika kipindi husika kulikuwa na jumla ya maombi 2,415 ya matangazo, mabadiliko na majibu ya hoja zinazohusu bidhaa tajwa ambapo 2,302 yalipokelewa katika mwaka 2017/18 na 113 ilikuwa ni baki

ya mwaka 2016/17. Maombi 2,260 (95%) yalifanyiwa tathmini ambapo 1,043 (46%) kati ya hayo yaliidhinishwa. Mchanganuo wa maombi hayo umeainishwa katika Jedwali Na. 2

Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa maombi mengine yanayohusu usajili wa bidhaa

Na	Aina ya bidhaa	Maelezo	Baki ya 2016/17	Pokelewa 2017/18	Jumla	Tathminiwa	Idhinishwa	Kataliwa	Baki
Dawa	Binadamu	Matangazo	4	194	198	174	143	12	24
		Mabadiliko	31	795	826	803	787	1	23
		Majibu ya Hoja	39	788	827	794	0	0	33
		Jumla ndogo	74	1,777	1,851	1,771	930	13	80
	Mifugo	Matangazo	0	0	0	0	0	0	0
		Mabadiliko	0	9	9	9	7	0	0
		Majibu ya Hoja	2	80	82	81	0	0	1
		Jumla ndogo	2	89	91	90	7	0	1
	Mitishambaa	Matangazo	0	0	0	0	0	0	0
		Mabadiliko	0	0	0	0	0	0	0
		Majibu ya Hoja	0	11	11	11	0	0	0
		Jumla ndogo	-	11	11	11	0	0	0
2	Majoribio ya dawa	Mabadiliko	19	19	38	19	0	0	19
		Majibu ya Hoja	9	9	18	9	0	0	9
		Jumla ndogo	28	28	56	28	0	0	28
3	Vipodozi	Matangazo	0	54	54	54	54	0	0
		Mabadiliko	0	44	44	44	31	0	0
		Majibu ya Hoja	0	0	0	0	0	0	0
		Jumla ndogo	0	98	98	98	85	0	0

3	Vipodozi	Matangazo	0	54	54	54	54	0	0
		Mabadiliko	0	44	44	44	31	0	0
		Majibu ya Hoja	0	0	0	0	0	0	0
		Jumla ndogo	0	98	98	98	85	0	0
4	Vifaa tiba na vitendanishi	Matangazo	0	6	6	6	5	1	0
		Mabadiliko	0	18	18	13	13	0	5
		Majibu ya Hoja	0	187	187	146	0	0	41
		Jumla ndogo	0	211	211	165	18	1	46
5	Vipukusi	Matangazo	0	0	0	0	0	0	0
		Mabadiliko	0	3	3	3	3	0	0
		Majibu ya Hoja	9	85	94	94	0	0	0
		Jumla ndogo	9	88	97	97	3	0	0
Jumla Kuu			113	2,302	2,415	2,260	1,043	14	155

(h) Maombi ya dawa ambayo hayajafanyiwa tathmini kulingana na umri wa

kupokea (Age analysis)

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018 jumla ya maombi 144

yalikuwa bado hayajafanyiwa tathmini kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali Na. 3

Jedwali Na.3: Mchanganuo wa maombi ya usajili wa bidhaa ambayo hayajatathminiwa

Na	Aina ya Bidhaa	Idadi ya siku kwa mujibu wa MHW*	Muda uliopita tangu maombi kupokelewa								JUMLA
			<50	51-100	101-120	121-200	201-250	251-300	301-360	>360	
1	Dawa za binadamu na mifugo zinazotengenezwa nchini	120	0	0	0	0	0	0	0	0	0
2	Dawa za binadamu na mifugo zinazotengenezwa nchi za nje	240	72	0	0	0	0	0	0	0	72
3	Vipukusi	200	0	0	0	0	0	0	0	0	0
4	Vipodozi	50	0	0	0	0	0	0	0	0	0
5	Vifaa Tiba -Daraja A	100	0	0	0	0	0	0	0	0	0
	Vifaa Tiba -Daraja B	200	0	0	0	0	0	0	0	0	0
6	Vitendanishi	200	72	0	0	0	0	0	0	0	72
JUMLA KUU		144	0	0	0	0	0	0	0	144	

MHW* = Mkatuba wa Huduma kwa Wateja wa mwaka 2016

1.1.1.2 Usajili wa maeneo na utoaji wa vibali vya biashara ya dawa, vipodozi, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyongeza

Usajili wa maeneo ya biashara ya dawa, vipodozi, vifaa tiba na bidhaa nyongeza ulifanyika ambapo kati ya maombi 4,894 ya usajili wa maeneo yaliyopokelewa, yote 4,894

(100%) yalitathminiwa ambapo maombi 4,731(96.67%) kati ya hayo yalisajiliwa baada ya kukidhi vigezo kama Ilivyoainishwa katika Jedwali Na.4.

Jedwali Na. 4: Maombi ya usajili wa maeneo na utoaji wa vibali vya biashara ya dawa, vipodozi, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyongeza

Na	Aina ya jengo	Baki ya Juni, 2017	Yaliyopokelewa		Jumla	Yaliyotathminiwa	Yaliyosajiliwa	Vibali viliyyotolewa	Kataliwa/Hoja	%yaliyokidhi vigezo
			Mapya	Huishaa						
1	Dawa	Viwanda vya ndani	0	4	8	12	12	7	2	0
		Maghala	2	62	79	143	143	142	142	2
		Duka la jumla la dawa (Binadamu)	4	21	98	123	123	118	118	5
		Duka la jumla la dawa (Mifugo)	1	14	71	86	86	83	83	3
		DLDM - mifugo	7	193	224	424	424	417	417	7
		Magari	1	29	14	44	44	43	43	0
		Jumla ndogo	15	323	494	832	832	810	805	17
2	Vipodozi	Viwanda	Vikubwa	1	3	7	11	11	7	3
			Kati	0	2	5	7	7	3	3
			Vidogo	3	26	3	32	32	22	10
		Maduka ya Jumla		1	114	154	269	269	244	22
		Maduka ya Rejareja		8	1,410	1,884	3,302	3,296	3,244	2
		Maghala		0	39	93	132	132	129	3
		Magari ya kubebaa vipodozi		1	17	6	24	24	23	0
		Jumla ndogo		14	1611	2152	3777	3771	3672	43

3	Vipukusi	Viwanda	Vikubwa	0	1	0	1	1	1	1	0	100
			Kati	0	0	0	0	0	0	0	0	NA
			Vidogo	0	1	0	1	1	0	0	1	0
		Maduka ya Jumla		0	0	0	0	0	0	0	0	NA
		Maduka ya Rejareja		0	0	0	0	0	0	0	0	NA
		Maghala		0	0	0	0	0	0	0	0	NA
		Jumla ndogo		0	2	0	2	2	1	1	1	50
4	Vifaa tiba	Viwanda	Vikubwa	0	1	0	1	1	1	0	0	100
			Kati	0	0	0	0	0	0	0	0	NA
		Maduka ya Jumla		8	126	147	281	277	246	246	31	89
		Maduka ya Rejareja		0	1	0	1	1	1	1	0	100
		Jumla ndogo		8	128	147	283	279	248	247	31	89
JUMLA KUU				37	2062	2793	4892	4882	4730	4724	91	97

Idadi ya maombi iliyotathiminiwa mwaka huu, ina ongezeko la maombi 1,347 (38%) ikilinganishwa na maombi 3,535 yaliyotathiminiwa kwa mwaka 2016/17. Vile vile, idadi ya maeneo yaliyokidhi vigezo na kusajiliwa imeongezeka kwa idadi ya maombi 1,411 (43%) kutoka 3,319 hadi 4,730 ikilinganishwa na maeneo yaliyosajiliwa mwaka 2016/17.

Ongezeko hili linatokana na juhudzi zilizofanywa katika kazi za udhibiti pamoja na kutoa elimu kwa wadau mbalimbali hususan wajasiriamali kuhusu utii wa sheria kwa hiari.

1.1.1.3 Ukaguzi wa viwanda na maeneo ya biashara dawa, vipodozi, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyongeza

Ukaguzi wa viwanda na maeneo ya biashara za dawa, vipodozi, vifaa tiba na bidhaa nyongeza Jumla ya maeneo 9,277 yanayojihusisha na biashara ya dawa, vipodozi, vifaa tiba na bidhaa nyongeza yalikaguliwa. Mchanganuo wa taarifa za ukaguzi kuhusu maeneo haya zimeainishwa katika Jedwali Na. 5.

Jedwali Na. 5: Ukaguzi wa viwanda na maeneo ya biashara za dawa, vifaa tiba na bidhaa nyongeza

Na.	Aina ya Biashara	Maeneo yaliyokaguliwa			Yaliyokidhi Vigezo			
		Yaliyosajiliwa	Yasiyosajiliwa	Jumla	Idadi	%		
1	Dawa	Viwanda vya nje	0	103	103	81	79	
		Viwanda vya ndani	12	2	14	4	29	
		Maghala (Binadamu)	12	2	14	12	86	
		Duka la dawa – Famasi	898	28	926	876	95	
		DLDM-Mifugo	354	102	456	381	84	
		Duka la dawa – DLDM	2,353	210	2,563	2,299	90	
		Duka la dawa – Mifugo	160	123	283	159	56	
		Magari ya kubebaa dawa	6	7	13	13	100	
		Zahanati	172	4	176	170	97	
		Vituo vya Afya	150	0	150	150	100	
		Hospitali	296	4	300	295	98	
		Jumla ndogo	4,413	585	4,998	4,440	89	
2	Vipod ozi	Viwanda	Vikubwa	4	2	6	4	67
			Kati	0	1	1	1	100
			Vidogo	5	32	37	6	16
		Maduka ya Jumla		111	39	150	121	81
		Maduka ya Rejareja		2,704	1,156	3,860	2,874	74
		Maghala		35	8	43	35	81
		Magari ya kubebaa vipodozi		13	4	17	16	94
		Jumla ndogo		2,872	1,242	4,114	3,057	74
		Vifaa tiba	Viwanda	0	19	19	17	89
			Kati	0	0	0	0	NA
		Maduka ya Jumla		87	53	140	92	66
		Maduka ya Rejareja		1	0	1	1	100
		Maghala		0	5	5	0	0
		Jumla ndogo		88	77	165	110	67⁸
		JUMLA KUU		7,373	1,904	9,277	7,607	82

Kwa mujibu wa Jedwali Na. 5, maeneo 7,607 (82%) kati ya yaliyokaguliwa yalikidhi vigezo ikilinganishwa na maeneo 6,332 yaliyokidhi vigezo mwaka 2016/17. Kiwango cha kukidhi vigezo kimeongozeka kwa 20% kutokana na juhudzi zilizofanywa katika kazi za udhibiti pamoja na kutoa elimu kwa wadau mbalimbali hususan wajasiriamali kuhusu kutii sheria kwa hiari.

1.1.1.4 Ukuzaji wa viwanda vya ndani

Katika jitihada za kujenga Tanzania ya viwanda na uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, Mamlaka iliratibu na kuandaa kikao cha kushawishi wawekezaji na wenye nia hiyo zaidi ya 438 ya kujenga viwanda vya kutengeneza dawa na vifaa tiba nchini ambacho kiliongozwa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji na matokeo yake walijitokeza wawekezaji 70 ambaa wameonesha nia ya kuwekeza katika maeneo husika na baadhi yao wameshaanza ujenzi ikiwa ni pamoja na kuwasilisha maombi ya usajili wa viwanda vyao TFDA.

Aidha kilifanyika kikao kingine na wamiliki wote wa viwanda vya ndani vya kutengeneza dawa hapa nchini kwa lengo la kuhimiza viwanda hivyo kukidhi

Viwango vya Utengenezaji Bora wa Dawa (GMP) sanjari na TFDA kuwapatia wataalam wao mafunzo mifumo bora ya utengenezaji dawaili wawezekutengeneza dawa ambazo ni bora, salama na zenyefanisi.

1.1.1.5 Kaguzi maalum

Mamlaka ilifanya kaguzi tatu (3) maalumu katika kanda ya mashariki, ziwa, kati na kaskazini kwa kuhusisha mikoa ya Dar es salaam, Mwanza, Arusha, Mara, Geita, Shinyanga, Dodoma, Morogoro na Singida. Kaguzi hizi zililenga kutambua na kuondoa sokoni dawa duni na bandia, vipodozi visivyosajiliwa na kukabiliana na biashara haramu mitandaoni.

Katika kaguzi hizi, jumla ya majengo 351 yaliyaguliwa kwa mchanganuo ufuatao; famasi za dawa za binadamu (67), famasi za dawa za mifugo tano (5), hospitali tatu (3), kituo cha afya kimoja (1), maduka ya dawa muhimu za binadamu (196), maduka ya dawa za mifugo matatu (3), zahanati moja (1), vituo vya dawa za mifugo/veterinary centers sita (6), maeneo ya biashara za mitando sita (6) na majengo ya vipodozi (36). Wakati wa kaguzi hizi dawa aina za *diclofenac sodium injection*, *Co-malather suspension*, *Penizen V powder oral solution* na *Ascillin (Ampicillin Trihydrate 250mg capsules* zilibainika kuwa

bidhaa duni. Kufuatia ukaguzi huo jumla ya majalada ya kesi 23 yaliyofunguliwa dhidi ya wahusika.

Mamlaka kwa kushirikiana na Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala pamoja na Jeshi la Polisi ilifanya operesheni maalum kufuatilia matangazo na matumizi ya vifaa tiba kinyume na taratibu katika maeneo yanayotoa huduma ya tiba asili na tiba mbadala katika mikoa 11 nchini. Jumla ya maeneo 151 yaliyaguliwa, vifaa tiba 395 vyenye thamani ya shilingi za kitanzania 51,116,000 na dola za kimarekani 2,768 vilikamatwa na majalada ya kesi 51 yaliyofunguliwa.

Vile vile, Mamlaka ilifanya ukaguzi wa majaribio 37 ya dawa katika vituo kumi vya majaribio ya dawa viliwyoko katika mikoa ya Mbeya (7), Dar es salaam (4), Kilimanjaro (4), Bagomoyo (4), Korogwe (4), Manyara (2), Dodoma (1), Mwanza (8), Kisarawe (1) na Handeni (2). Kwa mujibu wa kaguzi hizo majaribio yote ya dawa yaliyonekana kufuata taratibu zinazotakiwa. Watafiti walielekezwa maeneo ya kufanya kazi wakati wa usimamizi wa majaribio hayo ili kuweza kuendelea kulinda afya ya watafiti na washiriki pamoja na kutoa matokeo sahihi.

1.1.1.6 Udhibiti wa uingizaji nchini na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi.

Katika kipindi husika, Mamlaka ilipokea jumla ya maombi 12,000 ya kuingiza bidhaa nchini ambapo maombi 11,866 (99%) yaliidhinishwa na

wahusika kupewa vibali. Vile vile, kulikuwa na maombi 1,222 ya kusafirisha bidhaa nje ya nchi ambapo maombi 1,206 (99%) yaliidhinishwa. Vibali 5,743 vya kuingiza bidhaa nchini na tisa (9) vya kusafirisha bidhaa nje ya nchi vilikaguliwa katika vituo

vya forodha. Mchanganuo wa maombi na vibali vilivyotolewa kwa bidhaa za dawa, vipodozi, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyongeza umeainishwa katika Jedwali Na. 6

Jedwali Na. 6: Maombi ya vibali vya kuingiza nchini na kusafirisha bidhaa nje ya nchi

Na	Aina ya bidhaa	Yaliyopokelewa		Vibali vilivyotolewa		Vibali vilivyokaguliwa katika vituo vya forodha	
		Kuingia	Kutoka	Kuingia	Kutoka	Kuingia	Kutoka
1	Dawa	4,068	110	4,029	104	2,027	9
2	Malighafi - Dawa	519	0	506	0	268	0
3	Vipodozi	1,319	962	1,287	956	695	0
4	Malighafi – Vipodozi	1,185	0	1,177	0	578	0
5	Vipukusi.	0	0	0	0	0	0
6	Vifaa tiba	4,909	150	4,867	146	2,175	0
7	Vitendanishi	0	0	0	0	0	0
Jumla		12,000	1,222	11,866	1,206	5,743	9

Kwa kuzingatia Jedwali Na.6, upo umuhimu wa kuwa na mfumo wa kielektroniki (IMIS) katika vituo vya forodha kwa ajili ya kufuatilia na kutunza kumbukumbu za vibali vilivyokaguliwa katika vituo vya forodha.

1.1.1.7 Ufutiliaji wa ubora wa dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi

(a) Ufutiliaji wa dawa

Ufutiliaji wa ubora wa dawa na bidhaa nyongeza hufanyika ili kutambua ubora wa bidhaa hizo kwenye soko. Zoezi la uchukuaji sampuli kwa mujibu

wa Mpango unaotekelezwa mwaka 2017/18 lilifanyika kupitia ofisi zote za Kanda. Jumla ya sampuli 525 za dawa zilikusanywa na kuchunguzwa. Dawa zilizokusanywa ni dawa ya sindano ya Artemether (47), vidonge vya Telmisartan Hydrochlorothiazide (42), Glimepiride (28) pamoja na vidonge vya kutibu fangasi kwa wanawake aina ya Clotrimazole (Vaginal Pessaries) - 51. Upande wa dawa za mifugo ni dawa ya sindano Ivermectin 1% (50) na dawa ya mchanganyiko wa Sulfadimezine na Trimethoprime (55). Dawa zote zilifaalu uchunguzi wa awali

wa maabara na kuwasilishwa maabara kwa ajili ya uchunguzi wa kina.

Aidha, Sampuli za dawa za kutibu malaria (119), kifua kkuu (TB-58) na dawa za kufubaza makali ya virusi vya ukimwi (ARV-133) zilikusanywa chini ya mpango wa ufutiliaji unaofadhiliwa na Mfuko wa Dunia (Global Fund). Sampuli zote zilizokusanywa zilifaalu uchunguzi wa awali wa maabara. Sampuli 28 za dawa nyingine zikiwemo kapsuli za Amoxicillin, dawa zenye mchanganyiko za amoxicillin+clavulinic acid pamoja na trimethoprime+

sulfamethoxazole zilikusanywa na kuchunguzwa ubora wake kupitia Mpango wa Ufutiliaji wa Ubora wa Dawa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Taarifa za Mpango wa Ufutiliaji wa Ubora wa Dawa awamu ya V – VI (2016 – 2017) na awamu ya I - VI (2014 – 2017) ziliandaliwa.

(b) Ufutiliaji wa ubora wa vifaa tiba na vitendanishi
Mpango maalum wa kufutilia ubora, usalama na ufanisi wa vifaa tiba na vitendanishi kwa mwaka 2018-2022 uliandaliwa na kuidhinishwa. Jumla ya sampuli 266 za surgical sutures, sterile gloves, HIV rapid test kits, Malaria rapid test kits, syringes, syphilis rapid test na surgical blades zilikusanywa katika soko. Sampuli 151 za surgical sutures, sterile gloves, HIV rapid test kits na Malaria rapid test kits zimefanyiwa uchunguzi na matokeo yanaendelea kufanyiwa tathmini.

(c) Ufutiliaji wa ubora wa vipodozi
Mpango wa ufutiliaji wa vipodozi katika soko wa mwaka wa fedha 2017/18-2019/20 (Post marketing surveillance of cosmetic products) uliandaliwa na kuidhinishwa kwa ajili ya kutumika.

Mafunzo ya jinsi ya kukusanya sampuli za vipodozi chini ya mpango huu yalitolewa kwa maafisa ukaguzi dawa wa mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya na Dodoma. Jumla ya sampuli 256

za vipodozi katika mikoa hiyo zilikusanywa na kufanyiwa tathmini. Uchunguzi wa sampuli hizo katika maabara utakamilika robo ya kwanza ya mwaka 2018/19.

1.1.1.8 Ufutiliaji wa usalama na matukio yanayohusiana na dawa na vifaa tiba

(a) Usalama na matukio yanayohusiana na dawa

Taarifa 234 za madhara yanayohisiwa kusababishwa na matumizi ya dawa (Adverse Drug Reactions) yalipokelewa na kufanyiwa tathmini pamoja na kuhifadhiwa katika kanzidata (Vigiflow). Kati ya taarifa hizo, 46 zilipokelewa kupitia mfumo wa kielektroniki wa utoaji wa taarifa za madhara ya dawa na 188 zilipokelewa kwa kupitia fomu za njano. Aidha, taarifa 50 za usalama wa dawa zilizosajiliwa (Periodic Safety Update Reports) zilipokelewa na kutathminiwa. Vile vile taarifa 50 za matukio makubwa ya kiafya ziliripotiwa kutoka katika majaribio ya dawa yanayoendelea.

Taarifa zote za usalama wa dawa zilipotiwa na kwa ujumla hapakuwa na taarifa za usalama na madhara ya dawa zilizohatarisha afya ya wananchi kwa mwaka 2017/2018 kiasi cha kupelekea Mamlaka kuchukua hatua zaidi.

Kazi ya uhamasishaji juu ya utoaji wa taarifa za madhara ya ilifanyika katika mikoa ya

20 ikiwemo Kagera, Mara, Simiyu, Manyara, Mtwara, Pwani, Lindi, Kigoma, Tabora, Katavi, Singida, Dodoma, Morogoro, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mtwara, Mara, Pwani na Shinyanga. Jumla ya watumishi 59 wa afya walipewa mafunzo ya uwezeshaji (TOTs) na mafunzo maalum ya usalama wa dawa yalifanyika kwa watumishi 179 katika mikoa ya Kigoma (20), Tabora (20), Singida (20), Dodoma (20), Morogoro (20), Kilimanjaro (20), Songwe (20), Mwanza (20) na Iringa (19). Aidha jumla ya watumishi wa afya wapatao 1,253 walihamishwa juu ya utoaji wa taarifa za madhara ya dawa katika mikoa ya Kagera (72), Mara (106), Simiyu (62), Manyara (128), Mtwara (54), Pwani (250), Lindi (46), Singida (52), Kilimanjaro (26), Iringa (77), Katavi (170), Tanga (98) na Shinyanga (70).

(b) Usalama na matukio yanayohusiana na vifaa tiba

Uhamasishaji juu ya utoaji wa taarifa za matukio yatokanayo na matumizi ya vifaa tiba na vitendanishi ulifanyika katika mikoa kumi (10) ya Morogoro, Iringa, Kilimanjaro, Ruvuma, Singida, Dodoma, Manyara, Tanga, Mbeya na Lindi ambapo jumla ya watoa huduma za afya 1,031 walihamasishwa.

Jumla ya taarifa 24 zilipokelewa katika kipindi hicho na kufanyiwa tathmini ambapo matoleo tisa (vifaa tiba 1 na vitendanishi 8) yaliondolewa kwenye soko.

1.1.2 K U H A K I K I S H A USALAMA NA UBORA WA CHAKULA

Mamlaka inajukumu la kudhibiti usalama na ubora wa vyakula vinavyozalishwa, kuingizwa, kusambazwa na kuuzwa nchini kwa matumizi ya binadamu ili kulinda afya ya jamii. Kwa kipindi cha Julai, 2017– Juni, 2018, Mamlaka imetekeleza jukumu hilo kwa kufanya kazi

zifuatazo:-

1.1.2.1 Usajili wa bidhaa za chakula

Jumla ya maombi 2,462 ya usajili wa bidhaa za chakula yalipokelewa ambapo kati yake 2,081 yalikuwa mapya, 381 yalikuwa ya kuhuisha usajili na 109 yaliyobaki bila kufanyiwa tathmini kufikia tarehe 30 Juni, 2017 na hivyo kufanya jumla ya maombi yaliyohitaji kufanyiwa

tathmini katika kipindi hicho kuwa 2,571.

Kati ya maombi haya, maombi 2,329 yalifanyiwa tathmini ikiwa ni 91 % ya maombi yote yaliyokuwepo. Maombi 2,104 yaliidhinishwa, 141 yalikuwa na hoja na 84 yalikataliwa. Mchanganuo wa maombi yote yaliyopokelewa, tathminiwa na kuidhinishwa umeainishwa katika Jedwali Na. 7.



Jedwali Na. 7: Mchanganuo wa maombi ya usajili wa vyakula, mabadiliko katika vyakula vilivyosajiliwa, matangazo na lebo

Na.	Aina ya bidhaa	Maelezo	Baki 2016/17	Pokelewa 2017/2018	Jumla	Tathminiwa	Idhinishwa	Kataliwa	Hoja	Baki
1.	Chakula	Mapya	109	2081	2189	1973	1799*	82	134	108
		Kuhuishwa	1	381	382	356	305	2	7	25
	Jumla ndogo		110	2462	2571	2329	2104	84	141	133

*Baadhi ya maombi yaliyoidhinishwa, tathmini yake ilifanyika katika kipindi cha mwaka 2016/17,

Idadi ya maombi kwa ajili ya usajili wa bidhaa za chakula imeongezeka kutoka 2,045 katika kipindi cha mwaka 2016/17 hadi 2,462 ikiwa ni ongezeko la maombi 417 sawa na 20 %. Ongezeko hilo linatokana na kuimarika kwa shughuli za udhibiti na utii wa sheria bila

shuruti kwa wafanyabiashara .

1.1.2.2 Tathmini ya maombi ya matangazo ya biashara, lebo na mabadiliko ya usajili wa chakula


Mamlaka ilipokea pia maombi jumla ya maombi 181 yanayohusu matangazo ya biashara, tathmini ya lebo

na mabadiliko ya bidhaa zilizosajiliwa Maombi yote yalifanyiwa kazi ambapo maombi 136 yaliidhinishwa, 41 yalikuwa na hoja na sita (6) yalikataliwa. Mchanganuo wa maombi hayo umeanishwa katika Jedwali Na. 8 na Mchoro Na.2

Jedwali Na. 8: Maombi mengine yanayohusu usajili wa bidhaa za chakula

Na.	Aina ya bidhaa	Maelezo	Baki 2016/17	Pokelewa 2017/2018	Jumla	Tathminiwa	Idhinishwa	Kataliwa	Hoja	Baki	Maoni
1.	Chakula	Matangazo	0	14	14	14	9	4	1	0	
		Lebo	0	142	142	142	102	0	40	0	
		Mabadiliko	0	25	25	25	23	2	0	0	
	Jumla		0	181	181	181	134	6	41	0	

Mchoro Na. 2: Idadi ya maombi ya chakula yaliyokuwepo, yaliyotathminiwa na yaliyoidhinishwa



1.1.2.3 Maombi ya usajili wa chakula ambayo hayajafanyiwa tathmini kulingana na umri wa kupokea

(Age analysis)

Jumla ya maombi 133 ya usajili wa chakula yalikuwa hayajafanyiwa tathmini kufikia

tarehe 30 Juni 2018 kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali Na. 9.

Jedwali Na. 9: Mchanganuo wa umri wa maombi ya usajili wa chakula ambayo hayajatathminiwa kwa mujibu wa Mkataba wa Huduma kwa Wateja (MHW)

Na	Aina ya Bidhaa	Idadi ya siku (MHW)	Muda uliopita tangu maombi kupokelewa (siku)					
			≤40	41-50	51-100	101-200	201-250	JUMLA
1	Chakula kilichofungashwa	40	71	29	11	0	0	111
2	Vyakula kwa ajili ya mahitaji maalum ya lishe (<i>high risk foods for special nutritional purposes</i>)	50	12	10	0	0	0	22
	Jumla							133

1.1.2.4 Usajili wa maeneo na utoaji wa vibali vya biashara ya chakula

Katika kipindi husika, jumla ya maombi 6,767 ya usajili wa

maeneo ya biashara ya chakula yalipokelewa na maombi, 6,723 (99%) yalitathminiwa. Kati ya maombi yaliyotahminiwa, 6,294 (94%) yalikidhi vigezo. Mchanganuo wa maombi ya usajili wa maeneo ya biashara

ya chakula ikiwa ni pamoja na makundi ya viwanda vya chakula vilivyosajiliwa umeanishwa katika Jedwali Na.10 na 11.

Jedwali Na. 10: Maombi ya usajili wa maeneo na utoaji wa vibali vya biashara ya chakula

Na	Aina ya jengo		Baki kutoka Juni, 2017	Yaliyopokelewa		Jumla tathminiwa	Yaliyosajiliwa	Jumla vibali viliwyotolewawa	Kataliwa/ Hoja	% yaliyokidhi vigezo
				Mapya	Huishwa					
1	Viwanda	Vikubwa	0	9	115	124	124	115	117	5 93
		Kati	6	78	210	294	294	259	261	9 88
		Vidogo	58	350	342	750	706	584	585	103 83
	Jumla ndogo		64	437	667	1,168	1,124	958	963	117 85
2	Maghala		0	343	388	731	731	629	631	96 86
	Hoteli		4	158	323	485	485	425	428	31 88
	Maduka ya Jumla		9	1,170	1,535	2,714	2,714	2,706	2,706	1 100
	Maduka ya Rejareja		10	220	313	543	543	452	438	21 83
	Machinjio		1	10	4	15	15	13	13	2 87
	Magari		0	349	762	1,111	1,111	1,111	1,111	- 100
	Jumla ndogo		24	2,250	3,325	5,599	5,599	5,336	5,327	151 95
JUMLA KUU			88	2,687	3,992	6,767	6,723	6,294	6,290	268 94

Kwa mujibu wa Jedwali Na.10, kuna ongezeko la maeneo 653 (11%) ikilinganishwa na maombi 9,320 yaliyotathiniwa mwaka 2016/17. Aidha,

wastani wa kukidhi matakwa kwa maeneo yanayojihusisha na biashara ya ya chakula umeongezeka kutoka 65% kwa mwaka 2016/17 hadi

69% kwa mwaka huukutokana na ongezeko la wakaguzi, vitendea kazi na utoaji wa elimu kwa wajasiriamali.

Jedwali Na. 11: Mchanganuo wa makundi ya viwanda vya chakula vilivyosajiliwa kwa kipindi cha mwaka 2017/18

Na.	Ofisi ya Kanda	Viwanda vidogo (Small scale food)	Viwanda vya kati (Medium scale)	Viwanda vikubwa (Large scale)	Jumla
1.	Mashariki	75	10	4	89
2.	Kaskazini	42	18	3	63
3.	Ziwa	44	34	9	87
4.	Kusini	26	14	2	42
5.	Magharibi	21	24	0	45
6.	Nyanda za Juu Kusini	15	15	1	31
7.	Kati	57	14	9	80
JUMLA		302	145	28	437

1.1.2.5 Ukaguzi wa viwanda na maeneo ya biashara za chakula

Maeneo yanayojihusisha na biashara ya chakula ikiwemo viwanda vya uzalishaji na majengo ya kuuzia hususan maghala, maduka ya chakula, migahawa, mahoteli, machinjio

na magari ya kubeba vyakula hukaguliwa kila mara ili kuhakiki ubora wake, mifumo ya utengenezaji na mazingira ya uzalishaji, usambazaji, uhifadhi na uuzaaji na hivyo kuimarisha udhibiti wa ubora na usalama wa bidhaa za chakula.

Kwa mwaka huu, jumla ya maeneo 10,273 yanayojihusisha na biashara ya chakula yalikaguliwa ambapo maeneo 7,093 (69%) yalikidhi vigezo. Mchanganuo wa taarifa za ukaguzi kuhusu maeneo haya zimeanishwa katika Jedwali Na. 12.

Jedwali Na. 12: Ukaguzi wa maeneo ya biashara ya chakula

Na	Aina ya biashara	Yaliyokaguliwa			Yaliyokidhi vigezo		
		Yaliyosajiliwa	Yasiyosajiliwa	Jumla	Idadi	%	
1	Viwanda	Viwanda vidogo	672	942	1,614	849	52.6
		Viwanda vya kati	306	117	423	319	75.4
		Viwanda vikubwa	154	6	160	144	90.0
	Jumla ndogo	1,132	1,065	2,197	1,312	59.7	
2	Maghala	452	189	641	477	74.4	
	Hotel	435	136	571	450	78.8	
	Maduka Jumla	3,227	1,198	4,425	3,244	73.3	
	Maduka Rejareja	771	545	1,316	955	72.6	
	Machinjio	43	179	222	55	24.8	
	Bucha	462	249	711	437	61.5	
	Magari ya kubebbea chakula	170	20	190	163	85.8	
	Jumla ndogo	5,560	2,516	8,076	5,781	71.6	
JUMLA		6,692	3,581	10,273	7,093	69.0	

Idadi ya maeneo yaliyokaguliwa mwaka huu ni ongezeko la maeneo 953 (10%) ikilinganishwa na maeneo (9,320) yaliyokaguliwa mwaka 2016/17. Aidha, wastani wa kukidhi matakwa ya sheria kwa maeneo yanayojihusisha na biashara ya chakula umeongezeka kutoka 65% kwa mwaka 2016/17 hadi 69% kwa mwaka huu. Kuongezeka kwa idadi ya maeneo yaliyokaguliwa inatokana na kuongeza kwa idadi ya wakaguzi pamoja na vitendea kazi.

1.1.2.6 Ukaguzi wa viwanda vya kusindika vyakula nyongeza na maziwa ya watoto wachanga nje ya nchi

Jumla ya viwanda 15 vya kuzalisha vyakula kwa ajili ya

mahitaji maalum ya lishe (High risk foods for special nutritional purposes) vilikaguliwa. Viwanda viwili (2) ni vya maziwa mbadala ya watoto wachanga na vyakula vya kulikiza nchini Vietnam na Zambia na viwanda 13 vilikuwa vya kuzalisha vyakula nyongeza (food supplements) vilivyopo nchini India (4), Malaysia (4) na China (1). Viwanda vyote vilikidhi vigezo na bidhaa zinazozalishwa na viwanda hivyo zimesajiliwa.

1.1.2.7 Udhibiti wa uingizaji nchini na usafirishaji wa chakula nje ya nchi

Udhibiti wa uingizaji nchini na usafirishaji nje ya nchi wa bidhaa za chakula hufanyika ili kuhakikisha kuwa bidhaa zote za vyakula na malighafi

zinazotumika kutengenezea vyakula zinakidhi vigezo vya usalama na ubora.

Mamlaka ilipokea jumla ya maombi 10,467 (Maombi 8,314 ya kuingiza nchini chakula na 2,153 ni ya kusafirisha chakula nje ya nchi) ambapo 10,407 (Maombi 8270 ya kuingiza nchini chakula na 2,137 ni ya kusafirisha chakula nje ya nchi) yaliidhinishwa na vibali kutolewa. Kati ya vibali vilivyoidhinishwa na kutolewa, vibali 5,506 vilikaguliwa katika vituo vya forodha ambapo 4,753 ni vya kuingiza bidhaa nchini na vibali 753 vya kusafirisha vyakula nje ya nchi. Mchanganuo wa maombi ya vibali vilivyoidhinishwa umeainishwa katika Jedwali Na.13

Jedwali Na. 13: Maombi ya vibali vya kuingiza nchini na kusafirisha chakula nje ya nchi

Na	Aina ya bidhaa	Yaliyopokelewa		Vibali vilivyotolewa		Vibali vilivyokaguliwa katika vituo vya forodha	
		Kuingia	Kutoka	Kuingia	Kutoka	Kuingia	Kutoka
1	Chakula	6,059	2153	6029	2137	3,510	753
2	Malighafi - Chakula	2255	0	2241	0	1243	0
Jumla		8,314	2,153	8,270	2,137	4,753	753

1.1.2.8 Ufuatiliaji wa mabaki ya dawa za mifugo katika nyama na uchafuzi wa madini tembo na mabaki ya viuatilifu katika mboga za majani

Mamlaka ilifanya ufuatiliaji ili kubaini hali ya uchafuzi wa madini tembo (heavy metals) kwenye mboga za majani zinazolimwa

katika mkoa wa Dar es Salaam ambapo jumla ya sampuli 195 zilichukuliwa na kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara wa aina tisa (9) za madini tembo. Matokeo ya uchunguzi yalionesha uwepo wa uchafuzi wa viwango visivyovumilika vya madini tembo hususan risasi, chromium

na arsenic katika mboga za majani. Idadi na asilimia ya sampuli zilizokuwa na uchafuzi kwa kiasi kinachozidi kiwango kinachovumilika kwa aina ya madini tembo ni ilikuwa kama ifuatavyo; risasi 182 (93%), chromium 131 (67%), arsenic 120 (62%), zinc 29 (15%), zebaki

28 (14%), cadmium 17(9%), shaba(copper) 0(0%), manganese 0(0%) na nickel 0(0%).

Matokeo ya uchafuzi wa madini tembo kwa viwango visivyovumilika yamewahi kuripotiwa pia katika tafiti mbalimbali zilizokwishafanywa na taasisi za elimu ya juu katika mboga za majani, maji na udongo kutoka katika baadhi ya maeneo ya mkoaa wa Dar es Salaam. Kwa ujumla matokeo yote hayo yanaonesha kuwa kilimo cha mboga katika baadhi ya maeneo ya mkoaa wa Dar es Salaam ni hatarishi kutokana na uchafuzi wa madini tembo unaosababishwa

na uchafuzi wa mazingira hivyo kuna umuhimu wa kuchukua hatua.

Mamlaka ilifanya ufuatiliaji ili kubainihaliya uchafuzi wa mabaki ya dawa za mifugo (veterinary drug residues) kwenye nyama za kuku katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Arusha, ambapo jumla ya sampuli 432 za nyama za kuku zilichukuliwa kutoka kwa wafugaji na katika soko kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara. Vilevile, Mamlaka kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu ilikusanya jumla ya sampuli 1,124 za mbogamboga kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Iringa,

Morogoro, Mwanza na Arusha kwa ajili ya uchunguzi ili wa mabaki ya viuatilifu. Taarifa ya matokeo ya uchunguzi itatolewa katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2018/19.

1.1.2.9 Taarifa za madhara yatokanayo na matumizi ya chakula kisicho salama

Mamlaka kwa kushirikiana na wadau wengine ilishiriki katika uchunguzi wa milipuko ya magonjwa yaliyohusishwa na matumizi ya chakula kisicho salama katika maeneo mbalimbali nchini kama ilivyooneshwaa katika Jedwali Na. 14

Jedwali Na: 14: Matukio yaliyodhaniwa kusababishwa na ulaji wa chakula kisicho salama

Na .	Mlipuko	Wilaya	Idadi ya walioathiri ka	Sababu inayodhaniwa (suspected cause)	Matokeo ya uchunguzi wa kimaabara	Afua (intervention)
1.	<i>Acute Aflatoxicosis</i>	Kiteto na kilindi	Watu 24 waliugua na kati yao 13 (54%) walifariki.	Mahindi yaliyochafuliwa na sumukuvu aina ya <i>aflatoxin</i>	Sampuli za mahindi kutoka kaya zizoathirika na mlipuko zilikuwa na uchafuzi wa <i>aflatoxin</i> kwa kiwango kinachowenza kusababisha madhara ya afya.	Elimu kwa umma kuhusu mikakati ya kupambana na sumukuvu ilitolewa kwa wananchi
2.	<i>Cyanide poisoning</i>	Kigoma Vijijini	Watu 10 waliugua na mmoja kati yao kufariki.	Ulaji wa ugali ulioandaliwa kwa unga wa muhogo uliodhaniwa kuwa na kiasi kikubwa cha <i>cyanide</i> .	Sampuli za unga wa mhogo na mihogo iliyokaushwa zilichukuliwa na zinafanyiwa uchunguzi wa kimaabara na matokeo kuonesha kuwa zilikuwa na kiwango kikubwa cha kemikali ya <i>cyanide</i> .	Elimu kwa umma kuhusu kujiepusha ulaji wa mihogo yenyewe kiwango kikibwa cha <i>cyanide</i> .
3.	Mlipuko uliohusish wa na ulaji wa nyama ya mzoga wa ngo'ombe	Kiteto na Ngorongoro	Watu 155 waliugua baada ya kula nyama ya mzoga wa ngombe katika wilaya tajwa kati yao wanane (8) (5%) walifariki dunia.	Ulaji nyama wa za mifugo iliyokufa, nyama mbichi, isiyova vizuri na isiyokaguliwa.	Sampuli za nyama hazikupatikana wakati wa ufuatiliaji	Elimu kwa umma kuhusu kuepuka ulaji wa nyama ya mzoga au isiyopimwa na afisa mifugo

Aidha, Mamlaka iliandaa rasimu ya Mwongozo wa kukabiliana na matukio ya dharura yatokanayo na matumizi ya chakula kisicho salama (Response Plan in Food Safety Emergency) ili kuweka mfumo rasmi wa kushughulikia matukio ya dharura (mlipuko) yanayohusiana na matumizi ya chakula kisicho salama.

Sanjari na hatua hiyo, jumla ya wataalam wa afya 181 wa fani ya afisa tabibu, fundi sanifu maabara na afisa afya katika mikoa ya Ruvuma, Mwanza, Mbeya, Mara, Arusha na Kilimanjaro walipata mafunzo ili kuwajengea uwezo katika

kufuatilia na kukabiliana na magonjwa yatokanayo na chakula.

1.1.2.10 Ufuatiliaji wa bidhaa za chakula katika soko

Jumla ya sampuli 431 za chakula (159 siagi ya karanga na 272 unga mchanganyiko) zilichukuliwa kutoka Kanda zote za TFDA kwa lengo la kubaini hali ya usalama wake wakati zinapokuwa katika soko. Sampuli zilizochukuliwa zilifanyiwa uchunguzi wa kimaabara ambapo matokeo yanaonesha kuwa sampuli 147

(34%) zilikuwa na uchafuzi wa sumukuvu aina ya aflatoxin kwa kiwango kisichokubalika.

Kufuatia matokeo hayo, Mamlaka inajikita katika kutoa elimu juu ya udibiti wa sumukuvu kwa wajasiriamali wanaojihusisha na usindikaji wa bidhaa hizi. Aidha, Jumla ya sampuli 558 za vyakula vilivyoongezwa virutubishi zilichukuliwa kutoka kwenye soko na kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara. Matokeo ya uchunguzi yamechananuliwa katika Jedwali Na. 15

Jedwali Na. 15: Matokeo ya uchunguzi wa vyakula vilivyoongezwa virutubishi.

Bidhaa	Chanzo cha sampuli	Idadi zilizochunguzwa	Faulu (idadi)	Faulu (%)
Vyakula vilivyoongezwa virutubisho	Unga wa ngano	216	160	74
	Mafuta ya kula	252	106	42
	Chumvi	90	67	75
Jumla		258	333	60

Kwa mujibu wa Jedwali Na. 16 hapo juu 60% ya sampuli zote zilikidhi vigezo. Kufuatia matokeo haya, Mamlaka itaendelea kufanya ufuatiliaji kwa wazalishaji pamoja na bidhaa husika kwa lengo la kuhakikisha kuwa bidhaa zinakidhi vigezo vya usalama na ubora.

1.1.2.11 M k a k a t i wa kudhibiti sumukuvu (mycotoxins) katika chakula

Ili kuimarisha jitihada za udhibiti

wa usalama wa chakula nchini, hususan katika kukabiliana na tatizo la sumukuvu, elimu juu ya madhara yatokanayo na sumukuvu na njia za kudhibiti sumukuvu katika mazao ya chakula ilitolewa katika wilaya za Kiteto, Chemba na Kondoambazo ziliathirika na mlipuko wa sumukuvu pamoja na Soko la Kimataifa la Nafaka Kibaigwa ambalo huhusika na ununuzi, uhifadhi na usambazaji wa mahindi kwa kiasi kikubwa.

Jumla ya watu 9,550 katika vijiji

48 na shule 7 katika maeneo tajwa walipata elimu juu ya sumukuvu ambayo ilitolewa kwa njia ya miadhara katika vijiji, shule, masoko na mikusanyiko mbalimbali. Vilevile wananchi walipewa vipeperushi vyenye ujumbe juu ya sumukuvu na mabango yaliwekwa kwenye maeneo yanayofikiwa na watu wengi. Hali kadhalika, jumbe fupi zilizorekodiwa juu ya udhibiti wa sumukuvu (radio spots) zilirushwa kuitia vituo vya radio za kijamii ili kufikia wananchi wengi. Kwa ujumla,

elimu iliyotolewa imejenga uelewa wa sumukuvu katika sehemu kubwa ya jamii na imeweza kufikia wananchi wengi hivyo inatarajiwa kuwa itasaidia jamii kujilinda dhidi ya sumukuvu.

Vilevile, katika kuratibu mikakati ya kitaifa ya kudhibiti uchafuzi wa sumukuvu katika chakula, ulifanyika mukutano wa Kamati Endeshaji ya Kitaifa ya Udhibi wa Sumukuvu (National Steering Committee on Mycotoxins Control) ambayo TFDA ni sekretarieti. Kamati iliendelea kujadili na kutoa mapendekezo ya kufanikisha utekelezaji wa mikakati ya kitaifa ya kudhibiti uchafuzi wa sumukuvu katika chakula nchini.

1.1.2.12 Mafunzo kwa wasindikaji wadogo wa vyakula

Mamlaka kwa kushirikiana na taasisi nyingine za serikali hususan Shirika la Viwango nchini (TBS), SIDO na TANTRADE ilifanya mafunzo yanayohusu usalama wa chakula kwa wasindikaji wadogo wa

vyakula katika mikoa ya Geita, Ruvuma, Songwe, Tabora na Katavi ambapo jumla ya wasindikaji 467 walishiriki. Mafunzo hayo yalitanguliwa na ukagazi wa maeneo yanayotumiwa na wasindikaji hao katika kusindika vyakula ili kubaini changamoto zilizopo na kutoa ushauri wa namna ya kuboresha maeneo hayo ili kukidhi matakwa ya uzalishaji wa salama wa chakula.

1.1.2.13 Mafunzo ya wakagazi wa chakula

Jumla ya wakagazi 50 wa TBS na TFDA (makao makuu, ofisi za kanda na vituo vya forodha) walipewa mafunzo ya pamoja katika masuala mbalimbali yanayohusu udhibiti wa chakula, utaratibu wa kutoa alama ya ubora ya TBS na maadili ya ukagazi ili kujenga uelewa wa pamoja wa wakagazi kutoka taasisi hizi mbili. Mafunzo haya ni sehemu ya utekelezaji wa Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) kati ya TBS na TFDA.

Hali kadhalika, jumla ya wakagazi wapya wa chakula 29

kutoka TFDA Makao Makuu, Ofisi za Kanda na baadhi ya vituo vya forodha walipatiwa mafunzo kuhusu Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali inayohusiana na shughuli za ukagazi

1.1.2.14 Uteketezaji wa bidhaa zisizokidhi viwango vya ubora na usalama

Mamlaka huteketeza bidhaa za chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi ambazo hazikidhi vigezo vya ubora, usalama na ufanisi ili kuepusha bidhaa husika zisitumiwe na walaji. Bidhaa zinazoteketezwa zinajumuisha zile zinazoombewa kibali (voluntary disposal) na wateja wenyewe kutokana na kuisha muda wa matumizi na zilizokamatwa katika kagazi mbalimbali kwa sababu hazijasajiliwa, kuwa duni/bandia baada ya uchunguzi wa kimaabara au zinazokutwa kwenye maeneo ambayo hayajasajiliwa na TFDA. Uzito na thamani ya bidhaa zilizoteketezwa kati ya Januari -Machi, 2018 vimeainishwa katika Jedwali Na. 16.

Jedwali Na. 16: Mchanganuo wa bidhaa zilizoteketezwa kwa kutokidhi vigezo

Na	Aina ya Bidhaa	Mchanganuo			
		Zilivyotolewa taarifa		Zilivyokamatwa	
		Uzito (MT)	Thamani (TZS)	Uzito (MT)	Thamani (TZS)
1	Chakula	2,485.01	20,668,626,038.00	877.76	1,597,135,635.00
2	Dawa za Binadamu	144.98	3,962,980,483.33	5.11	133,640,200.00
3	Dawa za Mifugo	0.22	44,000,000.00	0.23	13,938,333.00
4	Vipodozi	-	-	9.97	117,758,383.00
5	Vifungashio vya vipodozi	-	-	0.15	163,890.00
JUMLA		2,630.20	24,675,606,521.33	893.22	1,862,636,441.00

